**Journal of Kiswahili and Other African Languages**
Vol. 2 No. 1 (2024): ISSN (Online): 2958-4914
DOI: https://doi.org/10.58721/jkal.v2i1.491
*Mtazamo wa Ki-Afrika katika Nadharia za Tafsiri*

# Mtazamo wa Ki-Afrika katika Nadharia za Tafsiri

**Hadija Jilala**
*Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, Tanzania*

**Uwasilishaji wa Makala**
*Pokelewa: 2024-01-27*
*Rekebishwa: 2024-04-02*
*Kubalika: 2024-04-05*
*Chapishwa: 2024-04-14*

***Maneno Muhimu***
Tafsiri
Ki-Afrika
Nadharia
Uafrika

**Jinsi ya Kurejelea Makala:**

Jilala, H. (2024). Mtazamo wa Ki-Afrika katika Nadharia za Tafsiri. *Journal of Kiswahili and Other African Languages*, 2(1), 31-40.

*Copyright © 2024*
BY NC SA

**Ikisiri**
Makala haya yanahusu Mtazamo wa Ki-Afrika katika Nadharia za Tafsiri. Inafahamika kuwa chimbuko la nadharia za tafsiri zilizopo ni nchi za Kimagharibi. Hata hivyo, katika nchi za Afrika taaluma ya tafsiri imepiga hatua kubwa ya maendeleo ikiwa ni pamoja na kuwa na wataalamu na wanataaluma wengi wa tafsiri, kufundishwa katika shule za sekondari, vyuo vya kati na vyuo vikuu. Pamoja na maendeleo hayo, mpaka sasa hakuna nadharia ya tafsiri iliyobuliwa kupitia mazingira, muktadha na utamaduni wa lugha ya Kiswahili kama lugha ya Ki-Afrika. Hivyo, makala haya yanalenga kujadili umuhimu wa kuunda nadharia za tafsiri kwa kutumia muktadha wa lugha za Ki-Afrika na kupendekeza hatua zitakazochukuliwa katika mchakato wa kuunda nadharia za tafsiri za Kiswahili. Makala yanajadili kwamba, pamoja na kuwapo kwa nadharia zilizoibuliwa na wanazuoni wa Kimagharibi, kuna umuhimu wa kuunda nadharia za tafsiri ambazo zimefungamana na muktadha, mazingira, mila, desturi, historia, lugha na utamaduni wa Ki-Afrika. Hii ni kwa sababu tafsiri hushughulika na lugha ambayo ni mali ya jamii yenye utamaduni mahususi. Hivyo, nadharia za tafsiri zilizofumbata mtazamo wa Ki-Afrika zitakuwa msingi, dira na mwongozo wa kinadharia na kivitendo katika kushughulikia tafsiri za matini mbalimbali za lugha za Ki-Afrika, hasa zinazohusu dhana za kiutamaduni na fasihi. Vilevile nadharia hizo zitakuwa ni suluhisho la matatizo na changamoto za tafsiri kiisimu, kisemantiki, kiutamaduni na kifasihi. Makala haya yanapendekeza kuwa nadharia za tafsiri zinaweza kuundwa kwa kutumia mbinu mbalimbali kama vile kuunda nadharia mpya, kuasili nadharia zilizopo na kuziboresha nadharia hizo.

## Utangulizi

Tafsiri ni desturi kongwe ambayo imekuwepo hapa duniani tangu binadamu walipoanza kuwasiliana kwa njia ya mdomo (Mwansoko, 1996). Desturi hii imeendelea kushika kasi pale binadamu walipoanza kuwasiliana kwa njia ya maandishi na pia kutangamana na kuhusiana kwa jamii mbalimbali ambazo zinatofautiana katika tamaduni, lugha, historia na itikadi zake (Mwansoko, 1996). Kihistoria tafsiri imekuwa ikitumika kama nyezo na daraja la kuwaunganisha watu na mataifa mbalimbali duniani. Pia imetumika kurahisha mawasiliano kwa kuwawezesha watu kuelewana na kufahamiana (Mwansoko, 1996). Hivyo, tunaweza kusema kwamba tafsiri ni daraja na nyezo ya mawasiliano na utangamano wa ulimwengu. Kupitia tafsiri, jamii za lugha na utamaduni tofauti zimeweza kuhusiana, kutangamana, kuwasiliana na kuelewana, kujifunza na pia kufahamu maarifa, ujuzi, utamaduni na fasihi za jamii zingine.

Shughuli za tafsiri katika mabara ya Ulaya, Amerika, Amerika kaskazini na Asia zimekuwa zikifayika kwa kipindi kirefu. Katika bara la Afrika, shughuli za tafsiri zimekuwa zikifanyika tangu kale (Baker & Saldanha, 2009; Mwansoko, 1996). Kwa mfano, Kusini mwa Jangwa la Sahara, shughuli hizi zinakadiriwa kuwa na umri "takribani sawa na mawasiliano kwa njia ya mdomo" (Baker & Saldanha, 2009: 313). Kwa mujibu wa Mwansoko (1996), katika ulimwengu wa Kiswahili, hususan Tanzania, shughuli hizi zimekuwa zikifanywa na wapenzi wa fani hizi bila uratibu maalumu tangu karne ya 18.

Kama taaluma mahususi, uga wa tafsiri umeanza kujichomoza na kuenea kwa kasi katika nchi mbalimbali duniani kote katika kipindi cha karne ya 19 na 20 (Moser-Mercer, 1997; Venuti, 2004; Pöchhacker, 2004a; 2009; Munday, 2012). Mwansoko (1996) anafafanua kuwa, tafsiri kama taaluma mahususi imekua na kuenea kwa kasi katika nchi mbalimbali duniani katika karne ya 19. Kama taaluma, umuhimu wake umejipambanua zaidi na kuifanya iwe ni taaluma ambayo inakua na kuhitajika zaidi katika tafiti, uchunguzi na uandishi. Maendeleo haya yameshika kasi zaidi katika karne ya 20 kutokana na maendeleo ya sayansi na teknolojia na kuongezeka kwa wimbi la utandawazi ulimwenguni.

Ingawa tafsiri ni taaluma kongwe duniani, bado inaelezewa kuwa ni taaluma changa katika nchi za Afrika Mashariki hususan Tanzania. Mathalani, Mwansoko (1996) anaeleza kuwa taaluma ya tafsiri ilianza kufundishwa nchini Tanzania katika miaka ya 1970 tu. Swali la kujiuliza ni je, hakuna umuhimu wa kuwa na nadharia za tafsiri za Kiswahili? Na kama upo nini kifanyike ili tuweze kuwa na nadharia za tafsiri za Kiswahili ambazo zitakuwa ni dira na mwongozo wa kutatua changamoto za tafsiri za lugha za Kiafrika.

Hivyo, ni dhahiri kuwa maendeleo ya tafsiri kama taaluma yalienda sambamba na kuibuka kwa nadharia ambazo zilianzishwa kwa lengo la kuzungumzia, kuchambua, kuchanganua na kutathmini kazi na mausala ya tafsiri. Baadhi ya nadharia hizo ni; nadharia za ulinganifu, nadharia ya skopos, nadharia ya mifumo mingi na nadharia ya mawasiliano. Chimbuko na asili ya nadharia hizo ni Mabara ya Ulaya, Amerika ya Kaskazini na Asia. Kama anavyofafanua Mpemba (2016) kuwa asasi nyingi za tafiti na mafunzo ya ukalimani na tafsiri ziko nje ya bara la Afrika, hususan katika Mabara ya Ulaya, Amerika ya Kaskazini na Asia, na bara la Ulaya ndilo linaloongoza kwa kuwa na asasi nyingi zaidi. Kwa sababu hiyo, shughuli nyingi za tafiti na mafunzo ya ukalimani na tafsiri pia zimekuwa zikifanyika barani Ulaya, Amerika na Asia, huku bara la Ulaya likiwa linaongoza. Maelezo ya Mpemba (2016) yanathibitisha kuwa tafsiri kama taaluma imepiga hatua kubwa katika mabara mengine ukilinganisha na bara la Afrika. Aidha, hili linadhihirisha kuwa nadharia nyingi za tafsiri zinachimbukia kutoka katika mabara tajwa kwa sababu katika maeneo hayo taaluma hii imepiga hatua kubwa zaidi ya maendeleo. Kwa mfano, Mpemba (2016) anasisitiza kuwa nadharia nyingi zinazotawala katika nyuga za ukalimani na tafsiri zinatoka katika bara la Ulaya. Kwa hiyo, ni nadharia chache sana zinazofahamika katika ulimwengu wa Kiswahili na ni nadharia chache zaidi ambazo zimeandikwa kwa Kiswahili.

Hoja hii ya Mpemba inashadidia hoja yetu kuwa mpaka sasa hakuna nadharia ambayo imechimbukia kutoka katika muktadha, mazingira, lugha na utamaduni wa Kiafrika hususan lugha ya Kiswahili. Hali hii inalifanya bara la Afrika lionekane ni Bara pokezi la maarifa, ubunifu, ugunduzi na uvumbuzi. Hoja hii pia inajenga msingi wa makala haya kuhusu umuhimu wa kuunda nadharia za tafsiri.

Kwa upande mwingine, tulibaini kuwa nadharia za tafsiri zilizopo zimeonekana kuwa na upungufu katika kushughulikia masuala ya tafsiri hususan matini za kiutamaduni na kifasihi. Hii ni kwa sababu matini za kiutamaduni na za kifasihi hubeba dhana na vipengele vya kiutamaduni ambavyo hujikita

katika mazingira, lugha na utamaduni wa jamii mahususi (Jilala, 2014 & 2018). Jilala (2014) anaeleza kuwa nadharia za tafsiri zina mapungufu katika kushughulikia masuala ya tafsiri za lugha ya Kiswahili kutokana na umbali wa kiisimu, kimazingira, kijiografia, kimuktadha na tofauti za lugha na utamaduni ulioziunda nadharia hizo. Kwa mfano, katika utafiti wake Jilala (2014) alibaini uwepo wa matatizo ya kutumia nadharia ya Skopos katika kutafsiri matini za kiutamaduni kutoka lugha ya Kiswahili kwenda Kiingereza. Katika kutatua upungufu wa kutumia nadharia ya Skopos, Jilala (2014) alikuja na suluhisho la kuunda Modeli ya Mawasiliano ya Kiutamaduni (MMK) kama suluhisho la matatizo na udhaifu wa nadharia ya Skopos katika kutafsiri dhana za kiutamaduni kutoka lugha ya Kiswahili kwenda Kiingereza. Hivyo, kuundwa kwa MMK, kunatoa hamasa na haja ya kuandika makala haya ambayo yamelenga kujadili umuhimu wa kuunda nadharia za tafsiri zinazotokana na muktadha, mazingira, lugha na utamaduni wa Ki-Afrika na kutoa mapendekezo ya nini kifanyike ili kuwa na nadharia za tafsiri za Kiswahili. Vilele MMK inatusaidia kutambua kuwa suala la kuunda nadharia za tafsiri ni jambo linalowezekana.

Kwa umahususi wake, makala haya yanahoji ni kwa nini tusiunde nadharia za tafsiri? Tuna lugha ya Kiswahili, ambayo ni lugha ya Ki-Afrika inayoweza kufumbata na kuelezea masuala mbalimbali ya kitaaluma kinadharia na vitendo.Tuna wataalamu wa tafsiri, watafiti na wabobezi katika uga wa tafsiri wanaoweza kutumia tafiti zao kuzalisha na kuunda nadharia za tafsiri za Kiswahili. Lakini pia makala haya yanajengwa na hoja kwamba kutokana na maendeleo ya sayansi na teknolojia ni wakati wa Bara la Afrika kuondoka katika dhana ya upokezi wa maarifa, ujuzi na teknolojia mbalimbali na badala yake kuwa ni chanzo cha maarifa, ugunduzi na uvumbuzi ili mataifa mengine yaweze kutumia tafiti zinazotokana na muktadha, mazingira na utamaduni wa Afrika.

Ieleweke wazi si lengo la makala haya kuzipinga ama kupinga matumizi ya nadharia za tafsiri zilizopo. Hoja na msingi wa makala haya umejikita katika kukuza na kuimarisha maendeleo na matumizi ya lugha ya Kiswahili katika taaluma, hususan tafsiri. Kuipa lugha hii nguvu ya kifalsafa na kinadharia ili iwe lugha ya ubunifu, uvumbuzi, ugunduzi, mapinduzi na ukombozi wa kifikra na kiutamaduni kwa jamii za Afrika. Kwa kufanya hivi, bara la Afrika litatoka katika sifa ya upokezi wa maarifa na ujuzi na kuwa chanzo na chimbuko la maarifa. Aidha, makala haya yanalenga kuwa chachu, kutoa ari, hamasa na motisha kwa wanazuoni na watafiti wa uga wa tafsiri kuona haja na umuhimu wa kufanya tafiti zitakazosaidia kuunda nadharia za tafsiri kwa kuzingatia muktadha na mazingira ya Ki-Afrika.

Hivyo, makala haya si tu kwamba yanalenga kuwatia shime na kuwahamasisha wanazuoni na watafiti wa masuala ya tafsiri kutumia tafiti, maarifa, ubunifu na uvumbuzi wao kuunda nadharia za tafsiri zitakazokuwa mwongozo na msingi wa kuelezea, kuchambua, kuhakiki, kutafsiri na kushughulikia aina mbalimbali za matini na za lugha tofauti, bali pia yanafumbua fikra na mtazamo wa wanazuoni hao kuona umuhimu na hitaji la kuwa na nadharia za tafsiri za Kiswahili.

**Dhana ya Nadharia**

Kwa mujibu wa Chesterman (2004), nadharia inaeleweka kuwa ni mkusanyiko au mfungamano wowote wa dhana, mawazo, kauli, taratibu na kanuni mbalimbali zilizopangwa kwa utaratibu mahususi ili zitumike kama kiolezo cha kuelezea jambo fulani, kuongezea welewa wa mtu kuhusu jambo hilo au kama mwongozo mzuri wa mtafiti wa kudadisia na kutatulia matatizo yake ya kiutafiti (taz. Mkude, 2008). Nadharia ni maelezo ya jambo kufungamana na vigezo vilivyowekwa au vinavyozalika kutokana na majaribio ya jambo hilo. Yaani, nadharia inaweza kutokana na mawazo yaliyoundwa kitambo na jopo la wataalamu au inaweza kutokana na usomaji makini wa kazi ya fasihi ya mtu binafsi.

Hivyo, nadharia ni wazo ambalo huibuliwa kama mwongozo kwa mfasiri, msomaji ama mchambuzi na katika kutoa majumuisho ya kazi fulani maalum. Aidha, ni wazo kuu, fikra kuu, mwongozo wa mtu au watu au jamii ya mahali fulani wakati fulani kwa lengo maalumu (Jilala, 2016). Nadharia humwongoza mtu kutenda jambo fulani kwa utaratibu mzuri. Kwa hiyo, nadharia ndiyo msingi mkuu wa kuweza kuelezea jambo fulani ili liweze kukubalika, kuaminika na kufanyiwa kazi na watu wa jamii husika ama taaluma ya fani husika. Kwa maana hiyo, kila fani ina dira inayoiongoza fani hiyo katika uchunguzi, uchambuzi na ufafanuzi wa fani ama taaluma ya fani husika. Ndiyo sababu tuna nadharia za isimu, fasihi, siasa, uchumi, sosholojia, utawala n.k. (Jilala, 2016 ; Mpemba, 2016).

**Nadharia za Tafsiri**

Nadharia katika tafsiri ni dira, kanuni, utaratibu ambao humwongoza mfasiri katika mchakato mzima wa kutafsiri na ama kuelezea na kutatua matatizo na changamoto za tafsiri. Mwansoko (1996) anafafanua nadharia ya tafsiri kuwa ni maelekezo kuntu juu ya vipengele anuwai vya kifasiri vinavyopaswa kuzingatiwa na kila mfasiri akabiliwapo na kazi ya kufasiri. Hii ina maana kwamba nadharia katika tafsiri ni maelekezo juu ya nini kinapaswa kufanyika na kuzingatiwa pale mtu anapokutana na kazi ya tafsiri. Kwa upande mwingine, Munday (2012) anasema, nadharia ni kanuni ama msingi wa kikanuni ambao humpa mwongozo mfasiri aweze kukabiliana na masuala ya tafsiri katika kazi yake (taz. Munday, 2012; Mpemba 2016).

Katika taaluma ya tafsiri zipo nadharia mbalimbali ambazo zimeibuka kutokana na malengo, mtazamo na mkabala tofauti. Kama anavyofafanua Munday (2012) kuwa tangu kuibuka kwa taaluma ya tafsiri mpaka sasa, kumekuwa na nadharia zenye mitazamo mikuu mitatu ambayo ni mtazamo wa kiisimu, mtazamo wa kimawasiliano baina ya pande mbili au zaidi zenye tamaduni tofauti, na mtazamo wa kiuchanganuzi kilongo. Kwa ujumla mitazamo hii mitatu inatofautiana katika msingi wa msisitizo kuhusu tafsiri. Kwa upande mmoja kuna nadharia zinazosisitiza ulinganifu (taz. kwa mfano, Nida, 1964) na kwa upande mwingine kuna nadharia zinazosisitiza uamilifu wa ujumbe kwa kuzingatia nia mahususi ya mawasiliano (Okal, 2012). Aidha, kuna nadharia zinazoiangalia tafsiri kama mfumo ndani ya mifumo mingine na zinazoiona kwa jicho la kifalsafa (Mpemba, 2016). Hata hivyo, si lengo la makala haya kuchambua nadharia za tafsiri zilizopo bali ni kujadili umuhimu wa kuunda nadharia za tafsiri kwa kuingiza mtazamo wa Ki-Afrika katika nadharia za tafsiri, na pia kupendekeza nini kifanyike ili kufikia lengo hilo.

Mwansoko (1996) anazichukulia nadharia za tafsiri kuwa zinafumbatwa na nadharia moja pana inayoitwa 'Nadharia ya Tafsiri' ambapo anaona kuwa nadharia hiyo inaweza kufasiliwa ama kwa mtazamo finyu au kwa mtazamo mpana. Wakati ambapo mtazamo finyu unaiona nadharia ya tafsiri kuwa inahusika na uchunguzi wa mbinu zinazofaa kutumika kufasiri kwa ufanisi matini ya aina fulani mahususi, mtazamo mpana unaiona kuwa ni jumla ya maarifa yaliyopo na yale yatakayopatikana baadaye kuhusu mchakato wa kutafsiri. Maarifa hayo yanajumuisha dhana, misingi na kanuni za jumla, miongozo, mapendekezo na vidokezo muhimu. Mpemba (2016) anaeleza kuwa nadharia za tafsiri na ukalimani hazina budi kufanya mambo muhimu matatu yafuatayo:

1. Kuonyesha mbinu za tafsiri na ukalimani zinazofaa kutumiwa na wafasiri na wakalimani katika kufasiri na kukalimani aina mbalimbali za ujumbe kwa utoshelevu.
2. Kuwapatia wafasiri na wakalimani misingi, kanuni, sheria, maelekezo na vidokezo mbalimbali vya jinsi ya kufanya shughuli za tafsiri na ukalimani.
3. Kueleza namna ya kushughulikia vipengele vidogovidogo kama vile toni, viimbo, msisitizo, matumizi ya viungo vya mwili katika mazungumzo, udondoshaji, viakifishi, hatimlazo na kadhalika.

Mambo hayo matatu muhimu yaliyobainishwa na Mpemba (2016) yamejikita katika nadharia za tafsiri na ukalimani. Kwa upande wake Mwansoko (1996) anabainisha mambo manne yanayopaswa kushughulikiwa na nadharia. Jambo la kwanza ni kubainisha tatizo, ambalo ni mlolongo wa shughuli za kifasiri zinazopaswa kufanywa kutokana na matini aliyo nayo mfasiri. Kama nadharia inalenga kuelezea tafsiri, basi nadharia hiyo itaeleza tatizo la tafsiri; Jambo la pili ni kuonyesha vipengele vyote vinavyopaswa kuzingatiwa katika utatuzi wa tatizo linalobainishwa. Jambo la tatu ni kuorodhesha taratibu zote zinazoweza kufanikisha tafsiri inayohusika. Na mwisho ni kupendekeza taratibu zinazofaa zaidi kutekeleza shughuli za tafsiri pamoja na mbinu za tafsiri zilizo mwafaka zaidi kwa matini mahususi au ujumbe mahususi unaoshughulikiwa.

Hivyo, kwa kuzingatia mawazo ya Mwansoko (2016) na Mpemba (2016), kwa umahususi tunaweza kusema kuwa nadharia ya tafsiri inapaswa ifanye mambo muhimu saba ambayo ni:

i. Kubainisha tatizo la tafsiri katika mchakato mzima wa tafsiri
ii. Kuonesha mbinu za tafsiri zinazofaa kutumiwa na wafasiri katika kufasiri aina mbalimbali za matini kwa ufanisi na utoshelevu ili kuhakikisha maana na ujumbe wa awali haupotei ama kuharibiwa.
iii. Kutoa misingi, kanuni, sheria, maelekezo, vidokezo na taratibu maalumu za kuzingatia katika mchakato wa tafsiri.
iv. Kueleza namna ya kushughulikia vipengele vidogovidogo kama vile toni, viimbo, msisitizo, udondoshaji, viakifishi, hatimlazo na kadhalika.
v. Kuwa ni mwongozo maalumu wa namna ya kutafiti, kuchambua na kuhakiki tafsiri na kazi za tafsiri.
vi. Kuelezea namna ya kushughulikia dhana za kiutamaduni za lugha na jamii mbalimbali ikiwemo tamathali za semi, misemo, nahau, methali na mitindo mbalimbali ya lugha
vii. Kushughulikia matini za kifasihi kwa ufanisi na utoshelevu kwa kuzingatia muktadha, lugha, utamaduni na mielekeo ya jamii mahususi.

**Mtazamo wa Ki- Afrika katika Nadharia za Tafsiri**

Suala la mtazamo wa Ki-Afrika katika taaluma mbalimbali za Kiswahili si jambo geni. Kwa mfano, katika miaka ya 1970 kulizuka vuguvugu la kuwa na fasihi ya majaribio ambayo inaingiza vipengele vya fasihi simulizi za Ki-Afrika katika fasihi ili kuchotarisha kazi za fasihi kama vile tamthiliya na riwaya (Mulokozi 1996; Senkoro, 2006; Samweli, 2013). Kutokea kwa vuguvugu hilo kulisababishwa na kuwepo kwa kanuni na taratibu za utunzi wa riwaya na tamthiliya ambazo zilitokana na nadharia, msingi na mikabala ya fasihi ya Magharibi. Kwa maelezo ya wataalamu kama Mulokozi (1996) na Senkoro (2006), lengo la kuzuka kwa mkondo huu lilikuwa ni kufufua fasihi ya Waafrika iliyoonekana kumezwa na kaida za uandishi wa Kimagharibi. Msingi wa mawazo ya Mulokozi (1996) na Senkoro (2006) umejengwa katika dhana kuwa mkondo wa kimajaribio ulilenga kuingiza vipengele vya fasihi simulizi ya Waafrika katika fasihi andishi ili kuipa asili ya Uafrika. Baadhi ya watunzi wa kazi za fasihi walioingiza vipengele vya fasihi simulizi ya Kiafrika katika fasihi ya Kiswahili ni Penina Mlama, Ebrahim Hussein, Ephrase Kezilahabi, Emmanuel Mbogo na wengineo. Kwa mtazamo na mwelekeo huo, tunaona ipo haja pia ya kuingiza mtazamo wa Ki-Afrika katika nadharia za tafsiri kwa kuunda nadharia za tafsiri zinazotokana na tafiti za lugha ya Kiswahili, utamaduni, mazingira, muktadha, historia na fasihi ya Kiswahili kama moja ya lugha za Afrika. Tunatambua kwamba tafsiri kama taaluma inaongozwa na nadharia za Kimagharibi kama tulivyoeleza hapo awali. Hivyo, tunaweza kusema kwamba, tafsiri kama ilivyokuwa kwa taaluma zingine imepokea kanuni na taratibu mbalimbali kutoka katika nchi za Kimagharibi. Kwa umahususi makala haya yanajadili umuhimu na mapendekezo ya nini kifanyike ili kuingiza mtazamo wa Ki-Afrika katika nadharia za

tafsiri kwa kubuni na kuzalisha nadharia za tafsiri ambazo zimefumbata misingi, kanuni na mielekeo ya Ki-Afrika.

Dhana ya Mtazamo wa Ki-Afrika kama inavyotumika katika makala haya inarejelea nadharia za tafsiri ambazo zimetokana na lugha, utamaduni, mazingira na muktadha wa Kiswahili kama lugha ya Ki-Afrika. Mjadala wa makala haya umejiegemeza kutumia lugha ya Kiswahili kama kielelezo cha Uafrika kwa sababu ni lugha iliyoenea na kuzungumzwa na nchi nyingi za Afrika na inatumika na kutambulika kama lugha ya kazi na mawasiliano katika taasisi na jumuiya za Afrika kama vile Umoja wa Afrika, Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika n.k. Vilevile ni lugha iliyopata hadhi kikanda na kimataifa kwa kutambuliwa na Shirika la Elimu, Sayansi na Utamaduni la Umoja wa Mataifa na kupewa siku ya kimataifa ya Kiswahili (Jilala, 2022). Hivyo, hadhi na nafasi ya Kiswahili kitaifa na kimataifa inatufanya tuone kuwa lugha hii ni kielelezo cha Uafrika. Kwa mantiki hiyo, Kiswahili ni lugha inayohitaji kupewa nguvu ya kitaaluma hususan katika uga wa tafsiri ambapo kama tuliyoona tangu zamani tafsiri ilitumika kama daraja na chanzo cha maarifa na utambuzi wa maarifa ya jamii mbalimbali duniani. Hivyo, kupitia tafsiri ya matini za lugha na utamaduni wa jamii zingine, itasadia kuibua, kukuza na kuendeleza maarifa na ugunduzi mpya kwa kutafsiri nyaraka na vitabu mbalimbali kutoka katika lugha zingine kwenda Kiswahili na kinyume chake. Kama ambavyo historia inavyotubainishia, tafsiri ilisaidia kupata maarifa mapya na kutambua malimwengu ya watu wengine kupitia tafsiri ya vitabu vyao vya fasihi na hata mandiko mbalimbali kama vile Biblia na Kurani. Wamishenari pia waliweza kufahamu kuhusu Afrika kupitia tafsiri ya maandiko yaliyokuwepo (Mwansoko, 1996).

Kwa ujumla taaluma ya tafsiri imepiga hatua kubwa ya maendeleo na pia inatumika katika maisha ya kila siku katika taasisi za kitaifa, kikanda na kimataifa. Kuongezeka kwa mahitaji ya wafasiri na shughuli za tafsiri katika mashirika na taasisi mbalimbali za Afrika kama vile Umoja wa Afrika, Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika, Jumuiya ya Afrika Mashariki na zinginezo kunathibitisha haja ya kuwa na misingi bora ya kinadharia na vitendo katika tafsiri. Hatua hii pamoja na mahitaji na maendeleo ya tafsiri yanatoa msukumo wa kujadili kwa nini tusiwe na nadharia za tafsiri zilizokitwa kwenye lugha ya Kiswahili?

**Umuhimu wa Mtazamo wa Ki-Afrika katika Nadharia za Tafsiri**

Kama tulivyoona hapo awali, nadharia yoyote ya tafsiri ina lengo la kumsaidia mfasiri kushughulikia kazi za tafsiri kwa ufanisi na utoshelevu. Swali ambalo lilongoza mjadala wa makala haya ni je, kuna umuhimu wa kuunda nadharia za tafsiri zinazotokana na muktadha, mazingira, mielekeo, lugha na utamaduni wa Ki-Afrika? Sehemu hii inaeleza ni kwa nini ni umuhimu kuunda nadharia za tafsiri za Kiswahili.

Kwanza, kuweka misingi na taratibu za kinadharia na vitendo katika tafsiri: kuingiza vipengele ya Ki-Afrika katika Nadharia za Tafsiri kutasaidia kuweka misingi ya kinadharia na vitendo katika kubainisha na kushughulikia matatizo na masuala ya tafsiri. Hii ina maana kwamba, kwa kuwa na nadharia ambazo zimeibuliwa na kujikita katika uhalisia wa kimazingira, kijiografia na kimuktadha wa Ki-Afrika zitasaidia kupunguza matatizo na changamoto za tafsiri kwa kuwapa wafasili na wahakiki wa tafsiri miongozo na taratibu zilizojikita katika uhalisia na uasili wa lugha za Ki-Afrika kiisimu, kifasihi na kimuktadha. Kwa mfano, ni rahisi kutumia nadharia za tafsiri za Kiswahili katika kushughulikia tafsiri za misemo, nahau, methali, tamathari za semi za Kiswahili na dhana za kiutamaduni kuliko kutumia nadharia zinginezo. Kwa sababu nadharia hizo zinaweza kufumbata utamaduni wa jamii ilioyoziunda.

Pili, kushughulikia changamoto na matatizo ya tafsiri: uundaji wa nadharia za tafsiri utasaidia na kuwawezesha wafasili kushughulikia na kutoa suluhisho la matatizo ya kisemantiki, kiisimu, kimuundo, kifasihi na kiutamaduni katika tafsiri. Kwa mfano, nadharia za tafsiri zitaongoza uteuzi wa mbinu na visawe vya dhana za kiutamaduni na kuonesha dira na mielekeo ya kuzikabili changamoto na matatizo ya tafsiri ili kuzalisha tafsiri toshelevu na bora.

Tatu, kukuza taaluma ya tafsiri: kupitia nadharia ambazo chimbuko lake ni lugha ya Kiswahili, zitasaidia kukuza taaluma ya tafsiri ndani ya Afrika kupitia ufundishaji, ujifunzaji na tafiti za tafsiri. Hii ni kwa sababu zitakuwa na uwezo wa kuchunguza, kuchambua, kuelezea na kujadili tafsiri za lugha za Kiafrika. Vilevile, lugha inayotumika ni lugha inayoeleweka na inayoweza kutatua matatizo ya jamii kwa sababu imetokana na jamii, historia, lugha, utamaduni na muktadha wa jamii husika. Aidha, taaluma ya tafsiri itaweza kukua kwa sababu wengi watasoma, kujifunza na kujenga uwezo wa stadi, maarifa na ujuzi wa tafsiri kupitia lugha yao.

Nne, kuimarisha na kufanikisha mawasiliano: tunatambua kuwa dhima ya nadharia ya tafsiri ni kuwa daraja la mawasiliano na kurahisisha mawasiliano baina ya jamii ya lugha na utamaduni tofauti. Hivyo, nadharia zitakazoundwa zitasaidia kuondoa vizuizi vya mawasiliano na kurahisisha mawasiliano baina ya jamii za Ki-Afrika kwa kurahisha tafsiri ya machapisho na nyaraka mbalimbali kutoka katika lugha za Ki-Afrika kwenda katika lugha ya Kiswahili na kinyume chake ili kufikia umajumui wa Kiafrika.

Tano, kukuza na kuendeleza lugha ya Kiswahili na lugha zingine za Ki-Afrika: Kubuni, kuunda na kuibua nadharia za tafsiri zilizofungamana na mtazamo wa Ki-Afrika kutasaidia kukuza lugha ya Kiswahili na kuendelea kuipa nguvu katika matumizi kwenye tafiti na taaluma. Pia, nadharia hizo zitasaidia kukuza Taaluma ya Tafsiri katika Kiswahili. Mtazamo wa Ki-Afrika katika nadharia za tafsiri utasaidia kukuza na kuendeleza lugha ya Kiswahili kama lugha ya umajumui wa Afrika. Vilevile, kupitia nadharia za tafsiri, itakuwa rahisi kutafsiri matini na nyaraka zilizoandikwa kwa lugha za Ki-Afrika na kuzifanya ziweze kuhifadhiwa na pia kuandikwa na kuchapishwa.

Sita, kushughulikia mbinu za tafsiri: kuingiza mtazamo wa K-Afrika katika nadharia za tafsiri kutasaidia kuunda nadharia zinazoweza kuelekeza mbinu, kanuni na misingi ya mchakato wa tafsiri iliyojikita katika desturi, mila, utamaduni, imani na mielekeo ya jamii. Nadharia hizo zitakuwa ni dira madhubuti katika kumwongoza mfasiri kuteua mbinu na visawe muafaka vya maneno ili kupunguza changamoto na matatizo ya tafsiri.

**Hitimisho**

Makala haya yamejadili kuhusu mtazamo wa Ki-Afrika katika nadharia za tafsiri. Katika mjadala wa makala haya tumeonesha ni kwa nini tunahitaji kuwa na nadharia za tafsiri ambazo zinatokana na lugha, utamaduni, muktadha na mazingira ya Ki-Afrika. Hivyo, katika harakati za kuipa nguvu lugha ya Kiswahili kama lugha ya umajumui wa Kiafrika tunahitaji kuipa nguvu ya kitaaluma kwa kufanya tafiti za kutosha na kuitumia lugha hii kama nyenzo ya ubunifu, uvumbuzi na ugunduzi katika kuzalisha maarifa mapya na nadharia mpya ambazo zitashughulikia tafsiri za lugha za Ki-Afrika. Aidha, makala haya yamejadili kuwa katika mchakato wa uundaji wa nadharia za tafsiri, zipo nadharia za tafsiri ambazo zinaweza kuasiliwa au kuboreshwa na kisha kutumiwa kama nadharia za tafsiri za Kiswahili. Kwa ujumla makala haya yanajadili kuwa, upo umuhimu mkubwa sana wa kuibua nadharia za tafsiri ambazo zimejikita katika muktadha, mazingira, lugha na utamaduni wa jamii za Kiafrika kwa sababu jamii lugha hutofautiana na kwamba muktadha, lugha na utamaduni wa jamii lugha fulani hauwezi kutumika kujadili kwa ufanisi mkutadha, lugha na utamaduni wa jamii lugha nyingine. Hii ni kwa sababu nadharia zilizopo zimeibuka kutoka katika jamii lugha ambazo

zina mwachano mkubwa wa kiisimu na kiutamaduni na lugha za Ki-Afrika. Hivyo, kutokana na hitimisho hili makala haya yanapendekeza mambo yafuatayo kama yanavyojadiliwa katika sehemu inayofuata.

**Mapendekezo**

Makala haya yamejadili kuhusu mtazamo wa Ki-Afrika katika Nadharia za Tafsiri na kuonesha umuhimu wa kuwa na nadharia za tafsiri zilizochimbukia katika lugha za Kiafrika hususan Kiswahili. Tayari tumeona kuna umuhimu wa kuwa na mtazamo wa Ki-Afrika katika Nadharia za Tafsiri. Je, nini kifanyike ili kuhakikisha tunaweza kuzalisha nadharia za tafsiri za Kiswahili? Katika kujibu swali hilo, sehemu hii inatoa mapendekezo ya nini kifanyike ili kuwa na nadharia za Tafsiri za Kiswahili.

i) Kuunda nadharia mpya: Makala haya yanapendekeza watafiti, wataalamu na wanazuoni wa tafsiri kuunda nadharia mpya ambazo zitaendana na muktadha, historia, utamaduni, imani na itikadi za jamii za Kiswahili. Uundaji wa nadharia mpya uende sambamba na tafiti za kina kuhusu tafsiri na masuala ya tafsiri ili kuibuka na nadharia ambazo zinapimika na kuthibitika katika kuchunguza, kuchambua na kujadili masuala ya tafsiri.

ii) Kuasili Nadharia zilizopo: Kama inavyofahamika, zipo nadharia mbalimbali ambazo ziliibuliwa kutokana na mtazamo na mikabala tofauti tofauti katika lugha mbalimbali. Hivyo, nadharia hizo zinaweza kutumika katika Kiswahili kwa kuziasili na kuzifanya zisawiri mazingira na muktadha wa lugha ya Kiswahili. Kwa mfano, tunaweza kuziandika nadharia zilizopo kwa lugha ya Kiswahili na kutumia mifano ya lugha ya Kiswahili katika mjadala na ufafanuzi wa nadharia hizo.

iii) Kuziboresha Nadharia: Kuziboresha nadharia zilizopo kwa kuingiza mtazamo wa Ki-Afrika ndani yake, kushughulikia mapungufu yake na hatimaye kuwa na nadharia iliyo bora inayoweza kushughulikia masuala ya tafsiri katika Kiswahili. Kwa mfano, Jilala (2014) katika utafiti wake wa Uzamivu aliweza kuboresha nadharia ya Skopos na kuunda modeli ya tafsiri aliyoiita Modeli ya Mawasiliano ya Kiutamaduni (MMK) ambayo ililenga kushughulikia tafsiri ya matini za kiutamaduni kutoka Kiswahili kwenda Kiingereza. Aidha, Jilala (2018) aliipima modeli hiyo ikiwa inaweza kutumika kama nadharia mpya ya kutafsiri matini za Kifasihi. Hivyo, ipo haja ya kufanya tafiti mbalimbali na hata kuendelea kuifanyia utafiti modeli hii ili kuona kama inaweza kuwa ni nadharia ya tafsiri ya Ki-Afrika.

iv) Kuandaa wataalam wa tafsiri ambao wamejikita katika ubunifu na uvumbuzi: Kuandaa wataalamu wa tafsiri ambao watajengewa misingi ya ubunifu na uvumbuzi katika maendeleo ya tafsiri. Kwa kutambua umuhimu wa ubunifu na uvumbuzi, wataalamu wa tafsiri wataweza kutumia mbinu za ubunifu na uvumbuzi katika kuibua masuala na nadharia mpya katika tafsiri. Aidha, kuwa na kizazi cha wataalamu wa tafsiri wenye stadi za ubunifu na uvumbuzi kitasaidia kuwa na watu ambao wanaweza kuhoji, kutafakari, kutathmini, kuibua na kuandaa mikakati mipya na mbinu mpya za tafsiri.

v) Kuimarisha mafunzo ya tafsiri: Kama ambavyo imebainishwa hapo awali na pia maelezo ya wanazuoni, taaluma ya tafsiri imepiga hatua kubwa katika nchi za Ulaya, Amerika na Asia. Vyuo, taasisi na shule nyingi za tafsiri zinapatikana na katika nchi hizo na hatimaye nadharia nyingi zimezaliwa katika nchi hizo. Hii ni kwa sababu nchi hizo ziliwekeza katika kutoa elimu na mafunzo ya tafsiri na hivyo kuibua wataalamu wenye uwezo wa kuhoji, kujenga hoja na maarifa mapya kuhusu tafsiri. Hivyo, ipo haja ya kuimarisha mafunzo ya tafsiri katika shule, vyuo vya kati na vyuo vikuu na taasisi zingine. Hii itasaidia kukuza maarifa ya tafsiri na kupata wataalamu wa tafsiri ambao wanaweza kuzalisha nadharia za tafsiri.

vi) Kuimarisha na kuwekeza katika tafiti, uandishi na uchapishaji: Kuwekeza katika tafiti za masuala ya tafsiri, uandishi na uchapishaji ni miongoni mwa mikakati inayoweza kusaidia kuunda na kubuni nadharia za tafsiri katika Kiswahili. Nadharia haitoki katika umbwe tupu bali ni matokeo ya utafiti na majaribio ya kisayansi ambayo yanapimika na kuthibitika. Ili kufikia hapo kama nchi tunahitaji kuwekeza katika tafiti, uandishi na uchapishaji ambao unaweza kuzalisha nadharia za tafsiri za Kiswahili. Uwekezaji unahitaji kuwepo na fedha ambazo zitawafadhili watafiti wa masuala ya tafsiri waweze kufanya tafiti za kina, waweze kuandika na kuchapisha makala, majarida na vitabu vya tafsiri.

vii) Kuimarisha Ujuzi, Maarifa na Matumizi ya Teknolojia katika tafsiri: Tafsiri kama taaluma imepiga hatua kubwa sana kiteknolojia. Zipo mashine mbalimbali ambazo zinatumika kutafsiri, na uundaji wa nadharia zake unafanyika katika nchi ambazo zimepiga hatua kubwa katika maendeleo ya sayansi na teknolojia, maarifa ya tafsiri na tafiti za tafsiri. Hivyo, kuna haja ya kuimarisha programu za tafsiri ili ziendane na mapinduzi ya sayansi na teknolojia. Kuhakikisha programu hizo zinafahamika kwa wafasiri wa Tanzania na wanazuoni wa tafsiri. Miongoni mwa programu hizo ni pamoja na Tafsiri ya Google, Tafsiri ya mashine, Google CAT na zingine za mfano huu.

**Marejeleo**

Baker, M. na Saldanha, G. (wah.) (2008). *Routledge Encyclopedia of Translation Studies*, Tol. 2, Routledge.

Chesterman, A. (2004). "Paradigm Problems?" katika Schäffner, C. (mh.) *Translation Research and Interpreting Research: Traditions, Gaps and Synergies*. Multilingual Matters Ltd, uk. 52-56.

Jilala, H. (2022). Jilala, H. (2022). Kiswahili katika Utalii: Umuhimu, Dhima na Nafasi yake katika Maendeleo ya Utalii Tanzania. Katika Peter, M & Duwe, E (Wah.). *Kiswahili katika Anga za Kimataifa*. TUKI.uk. 261-296

Jilala, H. (2018). Uhakiki wa Modeli ya Mawasiliano ya Kiutamaduni katika Tafsiri. Je ni Mkabala Mpya wa Nadharia na Vitendo? Katika Kandagor, M. (Mh). *Kiswahili na Maendeleo ya Afrika Mashariki*. TUKI, uk. 338-367

Jilala, H. (2016). *Misingi ya Fasihi Linganishi: Nadharia, Mbinu na Matumizi*. Daud Publishing Company Ltd.

Jilala, H. (2014). Athari za Kiutamaduni katika Tafsiri: Mifano kutoka Matini za Kitalii katika Makumbusho za Tanzania. Tasnifu ya Uzamivu (Ph.D Kiswahili) (haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Mkude, D. J. (2008). "Mwanasayansi, Istilahi na Utengenezaji wa Kamusi" katika Kiango, J.G. (mh.) *Ukuzaji wa Istilahi za Kiswahili.* TUKI, uk. 156-165.

Moser-Mercer, B. (1997). "Process Models in Simultaneous Interpretation" katika Hauenschild, C. na Heizmann, S. (wah.) *Machine Translation and Translation Theory*. Mouton De Gruyter, uk. 3-18.

Mpemba, T. (2016). Nadharia za Tafsiri na Ukalimani. Katika Jilala, H. (Mh.). *Nadharia za Tafsiri, Ukalimani na Uundaji wa Istilahi*. Daud Publishing Company Limited, Uk.18-50.

Munday, J. (2012). *Introducing Translation Studies: Theories and Applications*, Tol. 3. Routledge-Taylor & Francis Group.

Mulokozi, M. M. (1996). *Fasihi ya Kiswahili*. KAUTTU.

Mwansoko, H. J. M. (1996). *Kitangulizi cha Tafsiri: Nadharia na Mbinu*. TUKI

Nida, E.A. (1964). *Towards a Science of Translating*. E. J. Brill.

Okal, B.O. (2012). "Nafasi ya Tafsiri katika Taaluma ya Onomastiki: Uhakiki wa Mbinu Zake katika Tafsiri ya Toponomastiki" katika *Kiswahili: Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili*, Juz. 75. TUKI, uk. 27-42.

Vol. 2 No. 1 (2024): ISSN (Online): 2958-4914
DOI: https://doi.org/10.58721/jkal.v2i1.491


Pöchhacker, F. (2004a). *Introducing Interpreting Studies*. Routledge.

Pöchhacker, F. (2009). "Issues in Interpreting Studies" katika Munday, J. (mh.) *The Routledge Companion to Translation Studies*. Routledge-Taylor & Francis Group, uk. 128-140.

Samweli, M. (2013).*Tamthiliya ya Kiswahili: Kutoka Miviga ya Kidini Hadi Filamu*. MEVELI Publishers.

Senkoro, F. E. M. K. (2006). "Fasihi ya Kiswahili ya Majaribio: Makutano Baina ya Fasihi Simulizi na Fasihi Andishi," *Kioo cha Lugha*, juzuu na. 4, uk 22-38.

Venuti, L. (mh.) (2004). *The Translation Studies Reader*. Routledge.